

Julai 11, 2021

Kwa Jamii yetu ya JCPS,

Wiki iliyopita, Vituo vya Kuthabiti Magonjwa (CDC) vilitoa mwongozo mpya kwa wilaya za shule kote nchini ili kupingua kuenea kwa COVID-19. Waraka huo mpya unaeleza hatua za usalama zinazopendekezwa kwa shule. Baada ya kukagua maelezo mapya, tunataka kushiriki sasisho na nyinyi.

Mwongozo wa CDC unapendekeza barakoa kwa mwanafunzi au mfanyikazi yeyote ambaye hawajachanjwa kikamilifu wakiwa ndani ya mali ya shule. Kama matokeo ya pendekezo hili jipya na mwongozo unaotarajiwa kutoka Idara ya Afya ya Umma ya Kentucky, wanafunzi na wafanyikazi ambao hawajachanjwa kikamilifu lazima wavae barakoa ndani ya mali ya JCPS kuanzia Jumatatu, Julai 12. Barakoa hazihitajiki ukiwa nje ya mali ya JCPS.

Mwongozo kutoka kwa CDC pia unapendekeza barakoakwa kila mtu kwenye basi la shule, hata kwa wale ambao wamechanjwa. Kwa kuzingatia pendekezo hili jipya, wanafunzi na wafanyikazi wote kwenye basi zetu kwa programu ya msimu wa joto lazima wavae barakoa.

Sasisho hili la barakoa limewekwa katika wilaya nzima kwa wiki chache zijazo. Bodi ya Elimu ya Kaunti ya Jefferson (JCBE) itapiga kura kwenye mkutano wa bodi wa Julai 27 na kufanya uamuzi kuhusu mahitaji ya usalama ikiwa ni pamoja na barakoa kwa wanafunzi na wafanyikazi wasiochanjwa mwanzoni mwa mwaka wa shule wa 2021-22.

Wasiwasi wetu kwa wanafunzi wetu, familia zetu na wafanyikazi wetu umekuwa katikati ya kila uamuzi tumefanya unaohusika na COVID-19. Tumetumia, na tutazidi kutumia, mwongz kutoka kwa wataalam afya wa serikali na kitaifa kuhusu njia iliyo salama zaidi kwenda mbele. Asanteni kwakuw washiriki nasi katika wakati wa mabadiliko katika jamii yetu. Tutazidi kufanya kazi pamoja kwa wanafunzi wetu.

Kwa Dhati,

Shule za Umma za Kaunti ya Jefferson